LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# MUUNDO WA MAMLAKA YA MAHAKAMA TANZANIA

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# MUUNDO WA MAMLAKA YA MAHAKAMA TANZANIA

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

YALIYOMO

**SHUKRANI** .......... **5**

**DIBAJI** .......... **5**

**UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU7**

**1. UTANGULIZI** .......... **9**

**2. NINI MAANA YA MAHAKAMA?** .......... **9**

**3. CHIMBUKO LA MAHAKAMA** .......... **10**

**4. AINA ZA MAHAKAMA** .......... **10**

4.1.Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano .......... 13

4.2.Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .......... 13

4.3.Mahakama ya Hakimu Mkazi .......... 14

4.4.Mahakama za Wilaya .......... 15

4.5.Mahakama ya Mwanzo .......... 16

**5. Uwezo/Mamlaka ya Mahakama** .......... **17**

**6. Aina za Mamlaka/Uwezo** .......... **17**

6.1.Mamlaka ya Kiwango cha Thamani .......... 18

6.2.Mamlaka ya Awali .......... 19

6.3.Mamlaka Pekee .......... 20

6.4.Mamlaka ya Rufaa .......... 20

6.5.Mamlaka ya Mapitio .......... 20

6.6.Mamlaka ya Usimamizi .......... 21

6.7.Mamlaka ya Mlingano .......... 21

6.8.Mamlaka ya Ziada .......... 21

**7. HITIMISHO** .......... **23**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususani, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo,Bi. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kwambaraia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inaababisha watu wengi

kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET).

Makao makuu ya Kituo yapo Dar es Salaam ambapo pia kuna Kituo cha Msaada wa Sheria na Arusha kuna ofisi ndogo.

# MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# 1. UTANGULIZI

Katika kitini hiki tunaangalia muundo waMahakama katika Tanzania ili kumsaidia mtu yeyote aweze kutambua mamlaka mbalimbali za Mahakama, Baraza au Kamisheni ambalo anaweza kwenda ili kupata utatuzi au nafuu juu ya suala ambalo linamtatiza.

# 2. NINI MAANA YA MAHAKAMA?

Mahakama ni chombo katika mfumo wa utawala wa dola ambacho ni moja kati ya mihimili mitatu ya dola, mingine ikiwa ni Serikali na Bunge. Mahakama ina wajibu wakutoa tafsiri ya sheria za nchi.

Dola ina mihimili mitatu na kazi zake ni kama ifuatavyo:-

i. **Bunge** - Kutunga sheria na kuisimamia serikali;
ii. **Mahakama** - Kutoa fasiri za sheria za nchi; na
iii. **Serikali** - Kusimamia na kutekeleza sheria pamoja na kutunga na kusimamia sera.

Vyombo hivi vitatu vikifanya kazi kwa uhuru, kwa mipaka ya kiutendaji na kuheshimu shughuli za kila kimojawapo, bila kuingiliana, ndiyo huleta utawala wa sheria katika nchi husika.

## 3. CHIMBUKO LA MAHAKAMA

Kama ilivyo kwa Bunge na Serikali, Mahakama pia inachimbuko lake katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Katiba ndiyo sheria mama katika nchi zote duniani na katika nchi yetu pia. KATIBA hiyondiyo iliyoanzisha mamlaka mbalimbali za dola kwa ibara zifuatazo:-

- » Serikali (Ibara ya 34);
- » Mahakama (Ibara ya 107 A);
- » Bunge la Jamhuri ya Muungano (Ibara ya 62).

Kwa hiyo, Mahakama inaundwa na Katiba ya nchi, na kupewa majukumu ya kutoa haki inapokuwa inasuluhisha na kuamua masuala mbalimbali ya kisheria iliyopewa mamlaka kuyashughulikia.

## 4. AINA ZA MAHAKAMA

Kuna aina zifuatazo za Mahakama katika nchi yetu:

i. Mahakama zinazoanzishwa moja kwa moja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani:
   - » Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
   - » Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

- » Mahakama Kuu ya Zanzibar; na
- » Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

ii. Mahakama zinazoanzishwa na sheria ya Mahakama za Mahakimu ya 1984:


- » Mahakama za Hakimu Mkazi;
- » Mahakama za Wilaya; na
- » Mahakama za Mwanzo.

iii. Mahakama Maalum zinazoanzishwa na Sheria maalum kushughulikia masuala maalum:

- » Mahakama/Kamisheni ya Kazi;
- » Mahakama ya Watoto;
- » Mahakama Kuu ya Biashara;
- » Mabaraza ya Ardhi. n.k

Hivyo basi, Katiba na sheria nyingine zinapounda Mahakama au Mabaraza/Kamisheni huzipa au kuyapa mabaraza hayo nguvu za kushughulikia mambo kama yalivyo ainishwa bayana katika Katiba au sheria husika. Katika kutekeleza nguvu au mamlaka hayo, Mahakama hazina budi kuhakikisha kwamba zinatenda yale tu na katika mipaka ile tu ambayo sheria inatamka.

Kwa hiyo, iwapo Mahakama itaamua jambo nje ya mipaka ya mamlaka iliyopewa basi maamuzi yake yatakuwa ni batili kwani itakuwa sio kazi iliyoelekezwa kutenda. Ufuatao ni muundo wa Mahakama Tanzania:




Kwa kutazama jedwali hili, huku tukiweka msisitizo katika Tanzania Bara, unaweza kusema muundo wa Mahakama nchini ni huu ufuatao:

### 4.1. Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano

Mahakama hii ndio yenye mamalaka ya mwisho katika kutoa haki natafsiri ya sheria na ambayo ikishatamka hakuna Mahakama ya chini yake tena inayoweza kupinga au kwenda kinyume na maamuzi hayo. Hii ni Mahakama ya kumbukumbu. Mkuu wa Mahakama hii ni Jaji Mkuu wa Tanzania ambaye ndiye mkuu wa Mahakama ikijumuisha mahakama ya Rufani na Mahakama zote zilizo chini yake. Watu wanaoketi na kuamua mashauri katika Mahakama hii huitwa Majaji wa Mahakama ya Rufani.

Sheria zinazoainisha nguvu, uwezo, mamlaka na mwenendo wa Mahakama hii ni;

i. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;
ii. Sheria ya Mahakama ya Rufaa ya 1979;
iii. Kanuni za Mahakama ya Rufaa, 2009.

### 4.2. Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(Ikijumuisha Mahakama Divisheni ya Biashara, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi na Mahakama

Kuu Divisheni ya Ardhi)

Mahakama hii pia inaanzishwa na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiyo Mahakama ya chini kutoka Mahakama ya Rufani. Kiutendaji, Mahakama Kuu ndiyo Mahakama ya juu kwa Mahakama zote za chini yake katika utendaji wa kila siku na ni Mahakama ya kumbukumbu pia. Mahakama hii huongozwa na Jaji Kiongozi akikaa pamoja na Majaji wengine. Mamlaka ya Mahakama Kuu ni pamoja na kupokea rufaa kutoka Mahakama za chini yake, kusikiliza mashaurii ya madai na kesi za jinai ambazo imepatiwa uwezo wa kuzisikiliza kisheria na kutoa tafsiri ya sheria.

## 4.3. Mahakama ya Hakimu Mkazi

Mahakama hii imeanzishwana Sheria ya Mahakama za Mahakimu ya 1984. Sheria hii inatamka kwamba Jaji Mkuu anaweza kutangaza kuundwa kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi katika eneo fulani la kijiografia au kwa sababu ya masuala fulani maalumu. Kwa kawaida, Mahakama ya Hakimu Mkazi huonekana kama ni "Mahakama ya Mkoa.

” Tafsiri hii siyo sahihi, hatuna Mahakama ya mkoa Tanzania bali tuna Mahakama ya Hakimu mkazi. Nguvu za Mahakama hii zinapatikana katika sheria zifuatazo,

a. Sheria ya Mahakama za Mahakimu, 1984;
b. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Daawa, 1966;
c. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai 1985; na sharia nyinginezo.

## 4.4. Mahakama za Wilaya

Sheria za Mahakama za Mahakimu inaanzisha pia Mahakama za wilaya ambapo katika kila wilaya kunatakiwa kuwepo na Mahakama itakayokaliwa na hakimu wa wilaya. Hakimu wa wilaya ana mamlaka ya kusikiliza kesi zote za jinai ambapo mahakama imepewa mamlaka kusikiliza. Hata hivyo hakimu huyo hana mamlaka juu ya mashauri ya madai kama hana elimu ya kiwango cha shahada mpaka pale tu anapoteuliwa na Jaji Mkuu kuwa Hakimu mwenye mamlaka ya kusikiliza mashauri ya madai.

## 4.5. Mahakama ya Mwanzo

Sheria ya Mahakama za Mahakimu ya mwaka 1984, inaanzisha kwenye kila wilaya Mahakama ya Mwanzo ambayo huwa na mamlaka katika eneo la wilaya ilimoanzishwa. Mahakama hii huanzishwa kutokana na ukubwa wa eneo katika wilaya. Kiutendaji, aghalabu kila tarafa lazima iwe na Mahakama ya Mwanzo.Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo hufanya kazi wakisaidiana na Wazee wa Baraza wasiopungua wawili. Lugha inayotumika katika Mahakama hii ni Kiswahili na mamlaka yake ya awali ni kusikiliza mashauri ya daawa na jinai. Pia Mahakama za Mwanzo husikiliza mashauri yote ya mirathi yanayohusisha sheria za kimila na sheria za Kiislamu.

Mahakama ya Mwanzo ni Mahakama ya chini kabisa katika muundo wa Mahakama na ndiyo Mahakama ambayo jamii inaifikia kwa urahisi. Mamlaka ya Mahakama hii katika jinai na madai si makubwa lakini inasaidia jamii kufikia mfumo wa sheria katika mambo yaliyo ya msingi.

## 5. UWEZO/MAMLAKA YA MAHAKAMA

- Mamlaka katika masuala ya jinai;
- Mamlaka katika masuala ya madai.

Uwezo au mamlaka ya Mahakama huainishwa katika sheria iliyotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi. Katika misingi hii basi ndio tumeweza kupata aina nyingi za mamlaka kama zinavyotamkwa na sheria mbalimbali

## 6. AINA ZA MAMLAKA/UWEZO

Kuna aina mbalimbali za mamlaka, ambazo Mahakama hupewa na sheria zinazoanzisha mahakama hizo kwakuzingatia yafuatayo:

- Kiwango cha thamani ya mali/malipo inayodaiwa katika shauri husika;
- Aina ya tatizo kama ndoa, kazi, ardhi, mikataba, n.k.
- Eneo linalohusika;
- Uzoefu na utaalamu wa Mahakimu kama stashahada, cheti au shahada ya sheria.

Baadhi ya mamlaka hayo ni kama ifuatavyo:

Mamlaka ya kieneo hutolewa ili Mahakama kushughulikia masuala ambayo yamo ndani ya eneo ambalo Mahakama hiyo imeanzishwa.Kwa mfano, kama kosa la jinai limetokea kwenye wilaya ya Tarime, basi suala hilo litapelekwa katika Mahakama ya Mwanzo katika wilaya hiyo, kwa kuwa hapo ndipo shauri hilo lilipotokea. Vivyo hivyo, kama suala hilo linashughulikiwa na Mahakama ya Wilaya basi litapelekwa ama kwenye Mahakama ya Wilaya hiyo au kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi, kama wilaya hiyo ina Hakimu Mkazi.

## 6.1. Mamlaka ya Kiwango cha Thamani

Hii ni mamlaka ambayo kama Mahakama zinashughulikia kesi za madai kuna mipaka katika viwango vya pesa ambazo Mahakama inaweza kushughulikia.Kwa mfano,Mahakama ya Mwanzo, inaweza kushughulikia madai yasiyozidi shilingi milioni thelathini (3o,000,000/=) kwa mali inayohamishika na shilingi milioni hamsini kwa mali isiyohamishika (50,000,000/=); ila haina kikomo katika mashauri ya mirathi ya kiislamu na kimila.

Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi inashughulikia daawa isiyozidi shilingi milioni mia mbili (200,000,000/-) kwa mali inayohamishika na shilingi milioni mia tatu (300,000,000/=) kwa mali isiyohamishika.

## 6.2. Mamlaka ya Awali

Hii ni mamlaka ya Mahakimu ya kusikiliza shauri kwa mara ya kwanza. Hii ina maana kuwa suala hilo likipelekwa kwenye Mahakama ya juu bila kupitia pale katika Mahakama hii basi shauri hilo aidha hutupwa au hurudishwa likasikilizwe kwanza kwenye Mahakama yenye mamlaka ya awali ya kusikiliza shauri hilo. Mathalan, Mahakama ya Mwanzo ina mamlaka ya awali kushughulikia mambo yote ya sheria za mila na sheria ya Kiislamu. Kila shauri linalohusu mambo hayo likipelekwa Mahakama ya Wilaya kabla ya kupitia Mahakama ya Mwanzo litatupiliwa mbali au litarejeshwa likasikilizwe Mahakama ya Mwanzo.

### 6.3. Mamlaka Pekee

Mamlaka haya hupewa kwaMahakama fulani pekee kusikiliza masuala fulani na inapopewa mamlaka hii hakuna Mahakama nyingine inayoweza kusikiliza isipokuwa tu kama inasikiliza kupitia mamlaka hii.Mamlaka haya mara nyingi hupewa kwa mabaraza maalum au vyombo fulani kama kwenye sheria za kazi na ajira, sheria ya watoto, sheria za ardhi, sheria ya uhujumu uchumi, n.k.

### 6.4. Mamlaka ya Rufaa

Kila sheria inapotoa mamlaka kwaMahakama kusikiliza suala fulani, hutoa pia haki na maelekezo iwapo wahusika wasiporidhika maamuzi hayo. Rufaa hukatwa katika Mahakama ya juu zaidi ya ile iliyotoa maamuzi ya awali.

### 6.5. Mamlaka ya Mapitio

Mahakama ya juu hupewa mamlaka ya kupitia maamuzi ya Mahakama za chini kuona kama ziliamua katika misingi ya haki na mipaka ya sheria.

### 6.6. Mamlaka ya Usimamizi

Mahakama za juu katika kila ngazi hupewa mamlaka ya usimamizi na utendaji katika Mahakama zilizochini ya mamlaka zao.

### 6.7. Mamlaka ya Mlingano

Haya ni mamlaka ya aina moja yanayotolewa kwa mahakama zaidi ya moja. Mathalan, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi zote zinauwezo sawa katika kutoa maamuzi.

### 6.8. Mamlaka ya Ziada

Wakati fulaniHakimu Mkazi anaweza kupewa mamlaka ya ziada kusikiliza mashauri ambayo vinginevyo husikilizwa na Mahakama Kuu tu. Maamuzi ya Hakimu huyo yatachukuliwa kuwa ni maamuzi ya Mahakama Kuu, baada ya kuidhinishwa na Mahakama Kuu.

Baadhi ya sheria zinazotoa mamlaka ya Mahakama:-

i. Sheria za Mahakama za Mahakimu 1984;
ii. Sheria ya Mahakama ya Rufani 1979;
iii. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Daawa, 1966;

iv. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985;
v. Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16;
vi. Sheria ya Uhujumu Uchumi, 1984;
vii. Sheria ya Ushahidi, 1967;
viii. Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, 1998;
ix. Sheria ya Ndoa, 1971;
x. Sheria za Ardhi Na. 4/5 ya 1999;
xi. Sheria ya Mahakama ya Kazi;
xii. Sheria ya Juu ya Hali ya Watu, GN 219/63 GN 276/63;
xiii. Sheria ya Mabaraza ya Kata, 1985, n.k.

# 7. HITIMISHO

Katika kitini hiki tumeweza kujifunza mambo mbalimbali kama vile maana ya Mahakama, chimbuko la Mahakama, aina za Mahakama, Mahakama ya Rufani ya Tanzania, Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mhakama ya Mwanzo. Pia tumeweza kuona kuwa kuna Mahakama maalumu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inakaa pale tu kunapotokea tatizo kuhusu tafsiri ya Katiba juu ya jambo linalohusu Muungano.

Pia zingatia kuna mabaraza maalum ya mashauri ya Ardhi ambayo mahakama za kawaida hazina mamlaka na mashaauri hayo isipokuwa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Pia kuna Baraza/Kamisheni la usuluhishi na uamuzi la masuala ya ajira.

Ndugu msomaji, ni matumaini yetu kuwa kijarida hiki kimekupa ufahamu wa kutosha juu ya mfumo mzima wa Mahakama. Hii itakusaidia wewe binafsi, pia kushauri wengine wapeleke wapi mashauri yao ili haki iweze kutendeka.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV


*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*